



JAMHURI YA MUUNGAANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS, TAWLA ZA MIKOA NA
SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA USHETU



**TANGAZO LA MAOMBI YA UKODISHAJI MAGARI KWA AJILI
YA ZOEZI LA UCHAGUZI MKUU 28/10/2020.**

KWA WANANCHI WOTE

Tarehe: 22/10/2020

Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu inapenda kuwaalika watu binafsi, Makampuni, Mashirika na Taasisi zenye magari mazima na yenye uwezo wa kubeba vifaa vya Uchaguzi kutuma maombi ya ukodishaji magari yao kwa ajili ya shughuli ya Uchaguzi Mkuu wa Rais, Ubunge na Udiwani utakaofanyika tarehe 28/10/2020 kazi hii itakuwa ndani ya siku mbili (2). Magari yafuatayo ndiyo yatakayohitajika kwa kazi hii:

S/NA	AINA YA GARI	IDADI
1.	Fuso box body/yenye bomba na kufunika kwa turubai zito.	04
2.	Toyota landcruiser Hardtop/Pickup au Hillux single cabin	28

2. Maombi yote yazingatie masharti yafuatayo:-

- i. Maombi yatawasilishwa kwa **Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya wilaya ya Ushetu, S.L.P. 50 Kahama.**
- ii. Maombi yote yawe na jina, anuani ya mwombaji na namba za simu, pamoja na mahali ofisi zake zilipo au kazi liwe na jina na

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji, Nyamilangano - USHETU, S. L. P. 50, KAHAMA.
Barua pepe: ded@ushetudc.go.tz Tovuti: www.ushetudc.go.tz



- anuari ya mwombaji ,aidha aoneshe mahali ofisi zake zilipo au anavyoweza kupatikana (physical address).
- iii. Magari yote yanatakiwa kuwa na Bima na nyaraka zingine zinazohusiana na gari ambazo ni hai.
 - iv. Gari liwe zima na lenye uwezo wa kutembea barabara ya vumbi bila shida.
 - v. Gharama za mafuta na posho ya dereva zitagharamiwa na mmiliki wa gari(mkodishwaji).
 - vi. Gharama ya kukodisha gari ni Tshs 300,000/= kwa siku.
 - vii. Mwisho wa kupokea maombi haya ni saa 6:00 kamili mchana siku ya jumamosi tarehe 25/10/2020 katika ofisi ya Msimamizi wa Uchaguzi katika Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu mtaa wa Nyamilangano.
 - viii. Maombi ambayo yatachelewa kwa muda uliopangwa na yatakayotumwa kwa njia ya mtandao (e-mail) hayatapokelewa.
 - ix. Mwombaji atakaeshindwa kuzingatia masharti haya atakuwa amejiondoa mwenyewe kwenye mchakato mzima wa maombi haya.



Matomora A Michael
MKURUGENZI MTENDAJI





JAMHURI YA MUUNGAANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS, TAWLA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA
MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA YA USHETU

**TANGAZO LA ZABUNI YA KUTAFUTA FUNDI (LOCAL FUNDI) KWA AJILI YA
UJENZI WA WODI TATU KATIKA HOSPITALI YA HALMASHAURI YA
WILAYA YA USHETU.**

KWA WANANCHI WOTE

Tarehe: 17/09/2020

1. Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu inakaribisha maombi ya Zabuni kutoka kwa Vikundi mbalimbali vilivyo sajiliwa, watu binafsi (local fundi) wenye uwezo wa kufanya kazi kama inavyoonekana katika jedwali:-

NA.	NAMBA YA ZABUNI	KAZI HUSIKA
1.	LGA.162/2020/2021/ USHETU/W/01	Ujenzi wa wodi tatu katika Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu

2. Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya anatoa mwaliko wa kotesheni kwa ajili ya ujenzi wa wodi tatu Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu.
3. Unakaribishwa kuleta kotesheni yako yenye bei kwa kila kazi iliyoainishwa kwenye kitabu cha kotesheni ambacho kinapatikana ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji.
4. Waombaji wote kwa Vikundi mbalimbali vilivyo sajiliwa au watu binafsi (local fundi) wawasilishe barua ya utambulisho toka kwa Mtendaji wa kata au Kijiji kuthibitisha juu ya ufundi wao, awe na wadhamini wasiopungua wawili, waombaji wawe na Akaunti yoyote ya benki hasa ya NMB ili kuwahisha malipo yao, pia waombaji wanatakiwa kuonyesha uzoefu wa kufanya kazi za ujenzi wa majengo ya serikali na wawe tayari kuonyesha kazi hizo.
5. Mwombaji anakaribishwa kuleta kotesheni yenye bei kwa kila kazi iliyoainishwa kwenye kotesheni ya gharama zisihusishe vifaa kwa kuwa fundi atapewa vifaa vya ujenzi.
6. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu anaweza kukubali zabuni ya chini au ya juu kulingana na uchambuzi wa zabuni husika (Evaluation)
7. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 22/09/2020 saa 4.00 asubuhi ikifuatiwa na zoezi la kufungua zabuni litakalofanyika katika ofisi Manunuzi na Ugavi katika Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu mbele ya wazabuni wote au wawakilishi wao watakaohudhuria.

8. Maombi yote ya zabuni yatakayochelewa hayatapokelewa na hayatafunguliwa wala kusomwa hadharani mbele ya wazabuni au wawakilishi wao wala kufanyiwa tathmini.
9. Tangazo hili ni la siku 4 za kikazi tangu tarehe 17/09/2020 hadi tarehe 22/09/2020 kutoka siku ile ya tangazo na siku zisizo za kazi.
10. Waombaji watakaopenda kuomba Kotesheni wafike kupata Maelekezo zaidi katika Ofisi ya Manunuzi na Ugavi S. L. P 50 USHETU-KAHAMA
Siku za kazi kuazia 2:00 asubuhi hadi saa 9:30 alasiri
11. Maombi ya Kotesheni yaandikwe kwa herufi kubwa Yakionyesha aina ya ZABUNI na JINA LA ZABUNI husika na Yawekwe kwenye bahasha isiyo na mchoro wala jina.
12. Bahasha ifungwe kwa lakiri.

MICHAEL A. MATOMORA
MKURUGENZI MTENDAJI.